102/3

**KISWAHILI**

Karatasi ya 3

**FASIHI**

**JULAI 2015**

Muda : Saa 2½

# SHULE YA UPILI YA MANG'U

# MTIHANI WA MWIGO

# 2015

for more free revision papers visit: www.freekcsepastpapers.com

## Maagizo

1. Jibu maswali **manne** pekee.
2. Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki ; yaani : Fasihi Simulizi, Hadithi Fupi, Riwaya na Tamthilia.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
5. Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa **lugha ya Kiswahili**.
6. Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapa.
7. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba **kurasa zote** za karatasi hii **zimepigwa chapa** sawasawa na kuwa **maswali yote yamo**.

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE**

## SEHEMU YA A: USHAIRI

1. **LAZIMA**

Ng'e na wangu uwezo
Simame bila vikwazo
Na fikira mzomzo
Kuwa ninakosa guzo
Na nguvu za kusimama
La maana nikaseme
Zinazokana dhuluma
Jambo hilo laniuma
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

Ombe dunia ilivyo
Mambo ya wasema ndivyo
Na vyombo walivyonavyo
Hutasema vyenginevyo
Aridhi haina wema
Sivyo huthubutu twama
Vinazuia kalmia
Ila watavyokutuma
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

Juu hakuniegemi
Aridhini sisimami
Wala kati sichutami
Wapi nisimame mimi
Hewa inanisakama
Kwa hizo nyingi zahama
Hakuna tena nudhuma
Kutaja yalofichama?
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

Hamisi yumo mbioni
Hasikii habaini
La nyuma halibaini
Kwamba kuna uyakini
Juma pumzi ahema
Kazi kwa la kutazama
Na mbele kulomwandama
Uovu waweza koma
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

Mwajuma hata mwamboni
Mbio mabarabarani
Nyoyo zimeshika kani
Hata uwambie nini
Wenenda wenenda hima
Matumbo yawanguruma
Kunyang'anya na dhuluma
Hubaki kukutazama
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

Taishika njia moja
Kwa kila alo mhoja
Watambuzi wa vioja
Na siku itapokuja
Kwayo sivunji mtima
Ukweli utamsama
Pamoja tutafungama
Waongo wataungama
Nisimame wapi ili n'pate kusema?

a) Eleza ujumbe wa shairi hili (alama 2)

b) Mshairi ametumia uhuru wa kishairi kutosheleza mahitaji ya kiaruudhi. Eleza kwa kutolea mifano miwili (alama 4)

c) Fafanua muundo wa shairi hili (alama 3)

d) Andika ubeti wa kwanza kaw lugha nathari (alama 5)

e) Bainisha nafsineni katika shairi hili (alama 2)

f) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

g) Msahiri anamaanisha nini anaposema

I) Juu hakuniegemi. Hewa inanisakama (alama 1)

for more free revision papers visit: www.freekcsepastpapers.com

II) Ni mbinu gain ya lugha imetumika katika mshororo huu (alama 1)

## SEHEMU YA B: FASIHI SIMULIZI

***Jibu swali la 2 au la 3***

2.
a) Fafanua maana ya maigizo (alama 2)

b) Kwa nini watu huhitaji kuigiza? (alama 4)

c) Miviga ni nini? (alama 2)

d) Miviga ina faida na hasara zake. Thibitisha ukweli wa kauli hii (alama 6)

e) Kwa nini ngomezi huhesabiwa katika utanzu wa maigizo (alama 2)

f) Jadili udhaifu wa ngomezi kama mbinu ya kupitisha ujumbe (alama 4)

3.

Ah! Mama anayekula chakula peke yake
Ah! Mama kabla hajala
Ah! Mama anasema, "Niongolee mtoto"
Ah! Mama akimaliza kula,
Ah! Mama husema, "Nipe Mtoto"

a) Eleza utanzu na kipera cha utungo huu (alama 2)

b) Fafanua sifa nne za kipera ulichotaja hapo juu (alama 4)

c) Vitendawili vina sifa nyingi. Taja tatu (alama 3)

d) Methani zinaweza kuainishwa kwa vigezo tofauti. Eleza vigezo vyovyote vine (alama 8)

e) Nyisi zina sifa gain? Toa mifano mitatu (alama 3)

for more free revision papers visit: www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

**S. A Mohamed na K. Walikora: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

***Jibu swali la 4 au la 5***

4.
a) Jadili ufaafu wa anwani Shaka ya Mambo (alama 9)

b) Mwandishi Farouk Topan amefaulu sana katika kutumia mbinu ya taharuki. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano saba (alama 7)

c) Taja na ufanue sifa nne za Esther (alama 4)

5. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili nafasi ya mwanamke

a) Mke wangu (alama 8)

b) Mwana wa Darubini (alama 12)

## SEHEMU D: RIWAYA

K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea

Jibu swali la 6 au la 7

6.

a) Mwandishi Ken Walibora amefaulu sana katika kutumia mbinu ya kejeli. Fafanua ukweli wa kauli hii (alama 10)

b) Onyesha vile maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika riwaya ya kidagaa kimemwozea

7. "…….huyo ni hatari kwa usalama …… Lakini …..Hivyo ndivyo sheria isemavyo. Msiba wa kujitakia hauna kilio."

a) Eleza maktadha wa dondo hili (alama 4)

b) Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

c) Jadili jinsi msiba wa kujitakia unavyojitokeza kupitia kwa wahusika wafuatao

i) Fao (alama 4)

ii) Mtemi Nasaba Bora (alama 6)

iii) Majisifu (alama 4)

## SEHEMU YA E: TAMTHILIA

*T. Arege: Mstahiki Meya*

8.

a) Kwa nini Baraza la Cheneo haliwezi kuafikia malengo ya milenia (alama 7)

b) Vijana wa Cheneo ni silaha mikononi mwa Meya. Fafanua ukweli wa kauli hii (alama 5)

c) Onyesha jinsi mwandishi amefaulu katika kutumua mbinu ya jazanda (alama 8)

for more free revision papers visit: www.freekcsepastpapers.com